

SHERIA NA HAKI

Kwa kila Mwananchi



Iwe shauku

Toleo Na. 008

Jarida la kila miezi mitatu

Oktoba - Disemba, 2011

Zanzibar Kuanzisha 'Yearbook of Law'



Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) Prof. Chris Maina Peter akieleza mpango wa kuanzisha Zanzibar Yearbook of Law mbele ya Jaji Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Omar Othman Makungu. Wengine ni Kaimu Mkurugenzi ZLSC, Harusi Miraji Mpatani na Mjumbe wa Bodi Ali Uki.

UJUMBE wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) umefanya ziara rasmi ya kumtembelea Jaji Mkuu Zanzibar (JMZ) Mheshimiwa Omar Makungu na Mwanasheria Mkuu Zanzibar (MMZ) Othman Masoud Othman katika afisi zao.

Ujumbe wa ZLSC uliongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini Profesa Chris Maina Peter. Wajumbe wengine ni Kaimu Mkurugenzi ZLSC Harusi Miraji Mpatani na Mshiriki (*associate*) wa Kituo Ali Uki.

Madhumuni ya ziara ilikuwa ni kuwapongeza JMZ na MMZ kwa kuteuliwa kushika nyadhifa hizo za juu za Sheria na kuwaelezea mpango wa Kituo wa kuanzisha Kitabu cha Sheria cha Mwaka Zanzibar (*Zanzibar Yearbook of Law*).

Profesa Peter aliwaeleza JMZ na MMZ kwa nyakati tofauti katika afisi zao kwamba lengo la kuanzisha Kitabu hicho ni kuweka kumbukumbu za mambo muhimu ya sheria yanayotokea kila mwaka.

Inaendelea Uk. 3

Yaliyomo

Tumikieni Wananchi Kwa Moyo Mkunjuvu - Profesa Peter Uk. 3

Paralegals Wafanya Mitihani ya Kumaliza Mafunzo Uk. 4

Siku ya Adhabu ya Kifo Uk. 5

Haki ya Rufaa Kisheria Uk. 12

Sheria ya Mzanzibari Mkaazi Uk. 14

Jaji Msoffe Ahimiza Hifadhi ya Haki za Binadamu Uk. 20

ZLSC Yakutana na Wadau Wake



Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) Prof. Chris Maina Peter akizungumza na wadau wa (ZLSC) kutoka sehemu mbali mbali za Zanzibar katika Ukumbi wa Umoja wa Watu Wenye Ulemavu, Wireless, Kikwajuni.


KITUO cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kimekutana na wadau kutathmini utendaji kazi wa Kituo mwaka 2011 na kujadili Mpango Kazi mpya (*Strategic Plan*) 2012-2016.

Wadau walieleza kuridhishwa na utendaji kazi wa Kituo kwa mwaka 2011 na kupendekeza kuwepo juhudi zaidi za kuelimishwa wananchi kujua haki zao, sheria na jinsi ya kuzisimamia katika vyombo vya Sheria.

Inaendelea Uk. 3

SHERIA NA HAKI

Kwa kila Mwananchi



Iwe shauku

Toleo Na. 008

Jarida la kila miezi mitatu

Oktoba - Disemba, 2011

Jaji Msoffe Ahimiza Hifadhi ya Haki za Binadamu

JAJI wa Mahkama ya Rufaani ya Tanzania, Mheshimiwa January Henry Msoffe alisisitiza umuhimu wa kuheshimiwa haki za binadamu.

Alisema hayo alipokuwa akitoa hotuba katika sherehe za kuadhimisha siku ya haki za binadamu iliyofanyika Disemba 10, 2011 katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA).

Alisema kwamba haki za binadamu lazima ziheshimiwe na wanaohisi haki zao zimevunjwa au zinaelekea kuvunjwa wafungue kesi Mahkamani ili haki itendeke.

Alisema Marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 yaliyofanywa mwaka 2010 yamezuia nafasi ya wanaolalamika kuhusu haki za binadamu kwenda Mahkama ya Rufaani ya Tanzania kutafuta haki.



Jaji wa Mahkama ya Ruffaa Tanzania, Mheshimiwa January Henry Msoffe (wa pili kutoka kulia waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wafanyakazi wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) alipotembelea Kituo hicho mtaa wa Migombani, Zanzibar

Inaendelea Uk. 18

JMZ Atangaza Siku ya Sheria Zanzibar



Jaji Mkuu Zanzibar Mheshimiwa Omar Makungu akitoa hotuba katika siku ya kumbukizi ya Profesa Haroub Othman katika ukumbi wa SUZA, Disemba 3, 2011.

JAJI Mkuu Zanzibar (JMZ) Mheshimiwa Omar Makungu ametangaza kwamba Zanzibar itaadhimisha siku ya Sheria (Law Day) kila mwaka kuanzia mwaka wa 2012.

Ahadi hiyo aliitoa alipokuwa akizungumza katika Kumbukizi ya Marehemu Profesa Haroub Othman iliyofanyika Disemba 03, 2011, katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA).

Jaji Makungu alikuwa mgeni rasmi katika Kumbukizi iliyoandaliwa na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC). Kila Jumamosi ya mwanzo ya mwezi Disemba ZLSC inatathmini kazi za kitaaluma za marehemu Profesa Haroub na mchango wake katika jamii.

Inaendelea Uk. 18